

# KAIRUKI PHARMACEUTICALS INDUSTRY LTD

Incorporated in Kairuki Health and Education Network (KHEN)

192, Zegereni Industrial Area  
Kibaha Municipal  
Coast Region,  
P.O.Box 65300  
Tanzania



Tel: 255-22-2700021/4  
Mob: 255 717 171 500  
Email: kpil@kairukihospital.org

KPIL/KMT/1/20

26 Machi, 2020

Katibu Mkuu  
Ofisi ya Rais- TAMISEMI  
S.L.P. 1923,  
DODOMA.

## **YAH: OMBI LA KUTENGENEZWA BARABARA KATIKA ENEO LA VIWANDA ZEGERENI MKOANI PWANI**

Napenda kukufahamisha kwamba katika kuitikia wito wa Rais wa Jamhuri ya Muungano Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli wa ujenzi wa viwanda vya madawa nchini, kampuni ya Kairuki Pharmaceuticals Industries Limited (KPIL) imefikia hatua za mwisho za ujenzi wa kiwanda kwa asilimia 80% cha kuzalisha dawa za binadamu mkoani Pwani katika Wilaya ya Kibaha Vijijini. Kiwanda hicho mpaka kukamilika ujenzi wake kitagharimu takribani shilingi Bilioni 32 na kinatarajiwa kuanza uzalishaji wa dawa za aina mbalimbali ifikapo mwezi Septemba, 2020.

Kiwanda hiki kitatoa ajira za moja kwa moja kwa zaidi ya Watanzania 200 na ajira zisizo za moja kwa moja kwa zaidi ya watu 300. Shehena ya kwanza ya **Makontena** 45 kati ya 60 yatakayobeba mitambo kwa ajili ya uzalishaji wa dawa yataanza kuwasili nchini mwishoni mwa Aprili, 2020.

Ili kuwezesha mitambo hiyo kufika katika eneo la kiwanda, tunaiomba Serikali iwezeshe Barabara ya kuelekea Viwandani katika eneo la Zegereni Kibaha kupitika kwa urahisi. Hivi sasa, barabara hiyo imeharibika kiasi cha kutoweza kupitika kwa urahisi hususani kwa magari makubwa ya mizigo. Ombi letu limezingatia ushauri wa mhandisi wa Mitambo ya kiwanda unaohitaji mitambo hiyo kutopata mtikisiko wa aina yoyote wakati wa kupakiwa, kusafirishwa na kupakuliwa.

Barabara hiyo itakapotengenezwa itakuwa na manufaa makubwa kwa viwanda zaidi ya 15 ambavyo vimeanza uzalishaji wa bidhaa mbalimbali na vingine vingi vinavyoendelea na ujenzi. Manufaa mengine ya kiuchumi ni pamoja na kodi mbalimbali zitakazolipwa na kiwanda chetu pamoja na viwanda vingine vya eneo hilo, ajira na fursa zaidi zingine za kiuchumi na kwa pato la Taifa.

Ni imani yetu kwamba maombi hayo yatapokelewa vizuri.

Wako katika ujenzi wa Taifa,

Dk. Muganyizi Kairuki  
Kaimu Mkurugenzi Mkuu KPIL



**Nakala:**

1. Katibu Mkuu  
Wizara ya Viwanda na Biashara,  
S.L.P. 2996,  
Dodoma.
2. Katibu Mkuu  
Wizara ya Afya na Maendeleo ya Jamii  
Jinsia, Wazee na Watoto,  
S.L.P. 743  
Dodoma.
3. Katibu Mkuu,  
Ofisi ya Waziri Mkuu – Uwekezaji,  
S.L.P. 980,  
Dodoma.
4. ✓ Mkuu wa Mkoa Pwani  
S.L.P 30080  
Kibaha
5. Mkuu wa Wilaya Pwani  
S.L.P 30153  
Kibaha

*Ulipokelewa tarehe  
21/4/2020*